# Lugha kama Nyenzo Inayotumiwa na Viongozi ili Kutimiza Malengo Yao Nchini Tanzania na Kenya

*Fabiola Hassan[1] na Gladdys Kinara[2]*
*[1]Chuo Kikuu cha Dodoma*
*[1]Chuo Kikuu cha Kibabii*

**Ikisiri**

**Viongozi ni watu wanaoongoza watu au kikundi fulani cha watu. Viongozi hutumia mbinu za ushawishi ili kuwafanya watu wanaowaongoza kuelewa, kuamini na kisha kutekeleza jambo ili kutimiza malengo yao katika taasisi, shirika au nchi. Ili kushawishi watu kuelewa, kuamini na kutekeleza jambo, viongozi hutumia nyenzo mbalimbali zikiwamo rasilimali fedha, rasilimali watu, rasilimali muda, mikakati, mipango pamoja na lugha. Hivyo, makala haya yanahusu lugha kama nyenzo inayotumiwa na viongozi ili kutimiza malengo yao nchini Tanzania na Kenya. Malengo yake ni kudadavua aina ya lugha ya ushawishi inayotumiwa na viongozi pamoja na kueleza namna lugha hiyo inavyoshawishi wananchi ili kutimiza malengo ya viongozi. Data zilizotumika zilikusanywa kwa njia ya uchambuzi matini pamoja usaili. Data hizo zimechambuliwa kimaelezo na kisha kufasiliwa kwa kutumia misingi ya *Nadharia ya Balagha* ya Aristotle (367). Baada ya kufasili data hizo, matokeo yanaonesha kwamba aina ya lugha ya ushawishi inayotumiwa na viongozi ni hii ifuatayo: matumizi ya nafsi ya kwanza wingi, kaulimbiu, maneno ya kilugha, nahau/tamathali za semi/misemo, istilahi rasmi, lugha isiyo rasmi, takwimu, sifa faafu za kiarudhi, lugha ya kujiamini, lugha ya kujali na lugha ya motisha. Imebainika pia kwamba aina hii ya lugha hutumiwa kushawishi wananchi kwa kujinasibisha, kuaminisha, kuhamasisha, kutumainisha, kuunganisha na kuongeza motisha. Kutokana na matokeo haya, imehitimishwa kwamba lugha ni nyenzo ya ushawishi ambayo inafanya kazi kama nyenzo nyingine zinazotumika ili kufikia malengo ya uongozi nchini Tanzania na Kenya.**

**Maneno Muhimu:** *Lugha, Nyenzo, Uongozi*

**Utangulizi**

Lugha ni zaidi ya chombo cha mawasiliano (Kyeu, 2011 na Matinde, 2012). Hii ina maana kwamba jukumu la lugha si kueleza, kufafanua au kuarifu pekee, bali pia lugha hutumika kutimiza majukumu mengine kama vile kutenda na kushawishi. Tunakubalina na maelezo ya Kyeu (2011) na Matinde (2012) kwamba lugha ina majukumu mengi zaidi ya kueleza, kufafanua na kuarifu. Makala haya yanahusu namna lugha inavyotumika kama nyenzo chanya inayotumiwa na viongozi ili kufikia malengo yao ya kushawishi ili kuendelea kushika dola kwa njia zinazoleta athari za kujenga katika jamii. Lugha ni nyenzo yenye nguvu inayoweza kuunda maoni, kuelewesha jamii, kuhamasisha jamii, kuaminisha jamii, kuunganisha jamii na kisha kuifanya jamii kutekeleza maagizo au maelekezo wanayopewa na viongozi wao.

Lugha inafafanuliwa kama mfumo wa mawasiliano unaotumia maneno, ishara, na miundo ya kisarufi ili kuwasilisha maana (Kyeu, 2011; Matinde, 2012, Phillipo, 2018 na Hassan, 2021). Lugha inaweza kuwa ya kitaifa kama Kiswahili na Kiingereza, rasmi kama Kiswahili na Kiingereza na Kikabila kama zilivyo Kisukuma & Kihaya (Tanzania) na Kijaluo & Kiluhya (Kenya). Katika makala haya, lugha inayoshughulikiwa ni lugha yeyote yenya athari chanya, kama vile kukuza umoja, kuhamasisha maendeleo na kuimarisha mshikamano wa kitaifa. Aidha, hatujashughulikia lugha yenye athari hasi kama vile kusababisha migogoro, kujenga chuki, kudunisha na kutenganisha jamii. Nyenzo inarejelea zana inayotumika kwa makusudi ili kufikia lengo fulani (TUKI, 2019). Katika makala haya, lugha inachukuliwa kama nyenzo ya kimkakati inayowezesha viongozi kushawishi na kuhamasisha jamii kwa lengo la kutimiza malengo yao ya kuendelea kuaminiwa na kushika dola. Aidha, viongozi ni watu wenye mamlaka au ushawishi wa kisiasa (TUKI, 2019). Uhusiano wa dhana lugha, nyenzo na viongozi unatokana na ukweli kwamba viongozi hutumia lugha kama nyenzo chanya ya kuwasilisha

maono yao, kuhamasisha wafuasi, na kufikia malengo yao ya kuendelea kushika dola kwa njia zinazojenga jamii.

Katika makala haya, dhana ya viongozi inarewajelea Rais Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Rais William Samoei Ruto wa Kenya. Viongozi hao wametumiwa kwa sababu wao ni marais wa sasa walioshika dola katika nchi zao, wakiwa na jukumu la kuunda sera na kuathiri mwelekeo wa kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Wote wawili wanalenga kuendelea kushika dola, hasa katika muktadha wa chaguzi zijazo, ambapo Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kugombea tena Urais nchini Tanzania Oktoba 2025, na William Ruto anatarajia kuimarisha msimamo wake wa kisiasa nchini Kenya na kisha kugombea tena mwaka 2027. Nchi za Tanzania na Kenya zimechaguliwa kwa sababu ya uhusiano wao wa kihistoria, ikiwa ni pamoja na kuwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na mfanano wa mifumo yao ya siasa. Katika nchi zote mbili vyama vya siasa vina ushawishi mkubwa. Aidha, demokrasia katika nchi hizo inakabiliwa na changamoto za ushindani wa kivyama na migogoro ya kiitikadi. Uhusiano huu wa kihistoria na mifumo ya siasa inayofanana hutoa msingi mwafaka wa kulinganisha jinsi lugha inavyotumika na viongozi wake kama nyenzo chanya ya kutimiza malengo yao ya kuendelea kushika dola.

Tatizo la msingi linaloshughuliwa katika makala haya ni jinsi lugha inavyotumika kama nyenzo chanya na viongozi kufikia malengo yao ya kuendelea kushika dola, na jinsi matumizi hayo yanavyochangia maendeleo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi nchini Tanzania na Kenya. Makala inasisitiza athari chanya za lugha, kama vile kukuza umoja wa taifa, kuhamasisha maendeleo, na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa.

Tafiti tangulizi zimeonyesha kuwa lugha ni sehemu muhimu ya uongozi, hasa katika muktadha wa ushawishi wa kisiasa (Austin, 1962; Searle, 1969; Hudson, 1978; Lakoff na Johnson, 1980; Atikinson, 1983; Dallmary, 1984; Heritage, 1986; Maitland & Wilson, 1987; Wilson, 1990; Tanaka, 1992; Schaffner, 1996; Chilton & Schaffner, 1997; Bell, 1988; Chilton, 1998; Bizzell & Herzberg, 1990; Lakoff, 1990; Gastil, 1992; Beard, 2000; Fairclough, 2000; Ismailova na wenzake, 2000; Lopez, 2000; Mendal, 2001; Nick, 2001; Helmbrecht, 2002; Kovecses, 2002; Lum, 2002; Bugarski, 2004; Iwamoto, 2005; Seker, 2005; Bull & Fetzer, 2006; Pelinka, 2007; Carver & Pikalo, 2008; Kramsch, 2009; Opeibi, 2009; Tong & Cheung, 2011; Abuya, 2012; Ayemoni, 2012; Ahmed, 2013; Akinkurolere, 2013; Macagno, 2014; Michira, 2014; Balogun, 2015; Shah & Pathan, 2016; Menya 2017; Degani, 2018; Kaur & Shapii, 2018; Lin, 2019; Hager na wenzake, 2020; Marcowitz & Slovic, 2020; Scotto Di Carlo, 2020; Sovu, 2020; Ademi na wenzake, 2021; Sovu, 2021; Abdul, 2022; Xhemaili, 2022 na Rahmani & Saeed, 2024).

Watifi hawa pamoja na mambo mengine wanaeleza kwamba lugha ni nyenzo ya ushawishi inayotumiwa na wanasiasa ili kufikia malengo yao. Mathalani, Mills (1984) anaeleza kwamba wanasiasa hutumia msamiati au istilahi zinazowakilisha dhana fulani katika kampeni maalumu. Suala hili pia linaungwa mkono na Menya (2017) ambaye anaeleza kwamba wanasiasa hutumia msamiati maalumu ili kutimiza kusudi lao na kwamba maana ya msamiati wowote ule hudokeza kusudi la mnenaji na hulenga mwitikio chanya wa msikilizaji. Lengo la kufanya hivyo kuwashawishi wapigakura wawachague dhidi ya wapinzani wao. Vilevile, Sovu (2020) na Sovu (2021) anaeleza kwamba wagombea katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 nchini Tanzania walitumia mbinu ya uteuzi wa msamiati au istilahi maalumu pamoja na nafsi mbalimbali ili kuwashawishi wapigakura wao waweze kuwachagua dhidi ya wapinzani wao. Naye Michira (2014) anaeleza kuwa kutokana na kanuni kali za Tume ya Uchaguzi ya Kenya, wagombea walitumia lugha kama nyenzo ya kutimiza malengo yao ya kutaka kuchaguliwa wao dhidi ya wapinzani wao kwa wakwepa kutaja moja kwa moja majina ya wapinzani wao. Aidha, walitumia mbinu viwakilishi nafsi ‘sisi’ kujirejelea wao na ‘wao’ kurejelea wapinzani. Hivyo, ni wazi kwamba lugha inatumika kama nyenzo ya kutimiza malengo ya wanasiasa ya kutaka kushika dola au kuendelea kushika dola. Kuhusu nafasi ya lugha kwa viongozi, Fairclough (2000) anabainisha kuwa lugha inatumika kama "diski" inayodhibiti mawazo na mitazamo ya jamii kwa njia za kujenga ili kutimiza malengo ya viongozi. Kutokana na tafiti tangulizi, tunakubaliana na hoja ya Fairclough (2020) kwamba lugha inatumika kama nyenzo ili kutimiza malengo ya viongozi ya kuendelea kushika dola. Kwa hiyo, makala haya yanachangia

maarifa kuhusu namna lugha inavyotumika kama nyenzo ili kutimiza malengo ya viongozi waliopo madarakani nchini Tanzania na Kenya.

Umuhimu wa utafiti uliozaa makala haya unatokana na kuwapo kwa muktadha shindani wa kisiasa na migogoro ya kiitikadi nchini Tanzania na Kenya. Pia, huu ni wakati huu wa kidijitali ambapo mitandao ya kijamii kama *X*, *WhatsApp*, *Tiktok*, *Facebook* na *Youtube* inatumika kwa mwitiko mkubwa na kwa haraka sana. Kutokana na kuwapo kwa mazingira hayo ya kiushindani wa kisiasa, migogoro ya kiitikadi na matumizi mapana ya mitandao ya kijamii, uteuzi sahihi na wa kimkakati wa lugha chanya ni muhimu zaidi kwa viongozi ili kutimiza malengo ya kuendela kushika dola. Makala hay yana malengo mawili. Mosi, kufafanua aina ya lugha inayotumiwa na viongozi kama nyenzo ya kutimiza malengo yao ya kuendelea kushika dola. Pili, kueleza namna lugha hiyo inavyoshawishi wananchi ili kutimiza malengo ya kuendelea kushika dola. Data zilizotumika zilipatikana kwa methodolojia ya utafiti kama inavyofafanuliwa katika sehemu ifuatayo.

**Methodolojia ya Utafiti**

Data zilizotumika katika makala haya zilitokana na utafiti uliofanyika maktabani na uwandani katika Mkoa wa Dodoma nchini Tanzania na Kaunti ya Bungoma nchini Kenya. Maeneo haya yalichaguliwa kama viwakilishi vya maeneo mengine ambayo yangewawezesha watafiti kupata data zinazohusu aina ya lugha inayotumiwa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais William Samoei Ruto pamoja na athari ya lugha hiyo katika kuleta ushawishi kwa wananchi ili watimize malengo yao ya kuendela kushika dola nchini Tanzania na Kenya. Watafiti walitumia usampulishaji nasibu ili kupata hotuba za viongozi tajwa katika maeneo tofautitofauti na mada tofautitofauti. Pia, walitumia usampulishaji huu ili kuwapata watoataarifa ambao ni Watanzania na Wakenya. Kwa kutumia mbinu ya kutegemea fursa, watafiti walipata jumla ya hotuba 10 za Rais Samia Suluhu Hassan na 10 za Rais William Samoei Ruto. Hotuba hizo zilipatikana katika mtandao wa *Youtube* na nyingine zilipatikana kutoka kwenye tovuti za Serikali ya Tanzania na ile ya Kenya. Aidha, hotuba hizo zilitumika katika mbinu ya uchambuzi matini. Pia, kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kutegemea fursa, watafiti waliwapata jumla ya Watoataarifa 10 ambao ni Watanzania 5 na Wakenya 5. Watoataarifa hao walitumika katika mbinu ya usaili. Idadi wa hotuba 20 na Watoataarifa 10 ilifikiwa baada ya kupata data sahihi na toshelevu.

Katika mbinu ya uchambuzi matini, watafiti waliandaa mwongozo wa hojaji uliowataka kusikiliza na kusoma hotuba za viongozi tajwa na kisha kubainisha aina ya lugha inayotumiwa na viongozi tajwa. Aina ya lugha iliyohitajika katika mwongozo inajumuisha mbinu mbalimbali za kisarufi zinazotumiwa na viongozi hawa ili kuleta ushawishi wakati wakiwasiliana na wananchi wanaowaongoza. Baada ya kuandaa mwongozo huo, walisikiliza na kusoma jumla ya hotuba 20 za viongozi tajwa. Mbinu hii iliwawezesha kupata data zinazohusu aina ya lugha kama vile matumizi ya: nafsi, msamiati maalumu, takwimu, kaulimbiu na lugha za kienyeji. Mbinu ya hojaji ilihusisha watoataarifa 10 na ilifanyika baada ya kukusanya data kwa kutumia mbinu ya uchambuzi matini. Katika mbinu hii, watafiti waliandaa hojaji yenye sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilikuwa na nukuzi kutoka kwenye hotuba za viongozi tajwa. Nukuzi hizo zilikuwa na vipengele vilivyopigiwa mstari kama vile nafsi, msamiati maalumu, kaulimbiu na lugha za kienyeji. Sehemu ya pili ilikuwa na swali lililolenga kujua athari za vipengele hivyo kwa wasikilizaji. Athari hizo zilihusu hoja kama vile ushirikishwaji, ujinasibishaji, ushirikiano na matumaini. Baada ya kuandaa hojaji hiyo, watafi waliwaomba watoatarifa kujaza majibu kuhusu swali lililopo katika sehemu ya pili. Mbinu hii iliwawezesha watafiti kupata data kuhusu athari za matumizi ya aina ya lugha katika kuleta ushawishi kwa wananchi unaowazesha viongozi kuendelea kushika dola. Baada ya kukusanya data, uchambuzi wa data ulifanywa kitaamuli kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Aidha, baada ya kuchambua data, ufasiri wa data ulifanywa kwa kutumia *Nadharia ya Balagha* ya Aristotle (367, KK) kama inavyoelezwa hapa chini.

**Nadharia ya Balagha**

Nadharia hii iliasisiwa na Aristotle miaka ya 367, KK. Miaka ya 2000 nadharia hii ilipata umaarufu na matumizi makubwa sana. Nadharia hii inasisitiza namna ya kuwa msemaji mzuri ili kuleta ushawishi kwa hadhira inayokusikiliza. Ili kuwa msemaji mzuri, nadharia hii imejikita katika misingi

mitatu. Msingi wa kwanza ni kuwapo kwa maudhui shahihi kwa hadhira sahihi. Msingi wa pili ni matumizi ya mbinu nzuri za kiisimu katika ili kuleta ushawishi kwa hadhira inayosikiliza. Misingi wa tatu ni mpangilio sahihi wa maudhui. Msingi wa pili wa nadharia hii umetumika kufasiri data za makala haya zinazohusu aina ya lugha inayotumiwa na Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto ili waweze kuwasahiwishi wananchi na kisha kuendelea kushika dola nchini Tanzania na Kenya. Kwa hiyo, kwa kutumia msingi huo, tumeweza kufasili data zinazohusu matumizi ya mbinu za kiisimu kama vile: nafsi, msamiati maalumu, kaulimbiu, takwimu na lugha za kienyeji. Data kuhusu aina ya lugha inayotumiwa na viongozi na athari zake kwa wananchi zimewasilishwa na kujadiliwa katika sehemu ifuatayo.

**Lugha ya Viongozi na Namna Inavyoshawishi Wananchi**

Data zilizokusanywa zinaonesha kwamba viongozi wa Tanzania na Kenya, yaani Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto, katika muktadha shindani wa kisiasa na migogoro ya kiitikadi, ni mahiri wa kuteua na kutumia lugha chanya inayoleta ushawishi kwa wananchi. Sehemu hii inawasilisha na kujadili data zinazohusu masuala hayo kwa kutumia *Nadharia ya Balagha* ya Aristitole, miaka 367 KK.

***a) Matumizi ya Nafsi ya Kwanza Umoja***

Hii ni kategoria ya kisarufi ambayo inaeleza au kuonesha nafasi za wahusika katika hali fulani maalumu (VIDE-MUWA, 2018). Katika lugha ya Kiswahili kuna nafsi ya kwanza umoja na wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi (Hassan, 2021). Data zinaonesha kwamba viongozi hutumia nafsi ya kwanza umoja kama lugha ya ushawishi. Viongozi hao katika hotuba zao hutumia kiwakilishi *mimi*, kiambishi nafsi {*ni-*} au kimilikishi {*-angu*}. Lengo la kutumia nafsi ya kwanza umoja ni kuaminisha uimara wao katika uongozi. Aidha, wanadhihirisha kwamba wana uwezo mzuri wa kutekeleza majukumu na hatimaye kufikia maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla. Aina hii ya lugha huwashawishi wananchi na hatimaye hutekeleza masuala yanayohamasishwa na viongozi hao. Tazama Data Na. (1).

Data Na. (1):

i. **<u>Ni</u>**kaamua kufanya mageuzi, niliyemuweka nikamwambia sasa nakupa miezi sita, nione umefanya kama Kilimo walivyofanya.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Januari 30, 2024.

ii. Wakati tumechaguliwa, tulikuwa na changamoto nyingi. Ikawa ni lazima **<u>ni</u>**pange vile **<u>ni</u>**tayashughulikia…Ikawa ni lazima **<u>ni</u>**punguze changamoto za taifa.

**Chanzo**: Rais William Samoei Ruto, mkutano na waandishi wa Habari kuhusu ziara ya huko mlima Kenya.

Data Na. (1) inaonesha matumizi ya nafsi ya kwanza umoja katika maneno *nikaamua*, *niliyemuweka*, *nione*, *nipange*, *nitayashughulikia* na *nipunguze*. Viongozi hawa wametumia nafsi hii ili kudhihirisha uwezo wao wa kiuongozi katika kufanya maamuzi. Hivyo, wananchi wanaosikiliza wanashawishika kwamba kuamini kwamba kiongozi aliyewekwa na Rais, kile kinachoonwa na Rais, mipango inayopangwa na Rais, masuala yanayoshughulikiwa na Rais pamoja changamoto zinazopunguzwa na Rais hufanyika hivyo kwa sababu ya uwezo wao. Kutokana na imani hiyo, katika muktadha shindani wa kisiasa nchini Tanzania na Kenya, wananchi wanashawishika na kisha ku waamini marais wao. Matokeo haya yanafanana na Sovu (2021) ambaye anabaini pia kwamba wagombea katika kampeni za uchunguzi mkuu nchini Tanzania mwaka 2015 walitumia pia nafsi ya kwanza umoja ili kuaminisha wapiga kura. Kwa hiyo, nafsi ya kwanza umoja ni aina ya lugha inayotumika na viongozi ili kuwashawishi wananchi kwa kuwaaminisha kwamba wao kama viongozi wanaweza uongozi.

***b) Matumizi ya Nafsi ya Kwanza Wingi***

Data zinaonesha kwamba nafsi hii inawakilishwa na kiwakilishi *sisi*, kiambishi nafsi {*tu-*} na kimilikishi {*-tu*}. Imebainika kwamba kiongozi hutumia nafsi ya kwanza wingi ili kudhihirisha

kwamba yeye pia ni sehemu ya jamii au jambo fulani la jamii. Aina hii ya lugha hushawishi wananchi na hatimaye hukubali au hutekeleza suala linalohamasishwa. Tazama Data Na. (2).

Data Na. (2):

i. **Tu**nataka kuwa na nchi ya kidemokrasia ya Kenya mahali maoni ya kila mtu ni muhimu.

**Chanzo**: Rais Dkt. William Samoei Ruto baada ya kuapishwa na mahakama ya Juu kuwa Rais Mteule wa 5 wa Kenya.

ii. Leo nitagusia baadhi ya masuala makubwa yaliyojiri mwaka tunaoumaliza, changamoto **tu**lizokabiliana nazo na **tu**nayoyatarajia mwakani 2025.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

Data Na. (2) inaonesha matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi {*tu*} katika maneno *tunataka*, *tulizokabiliana*, *tunayotarajia*, *tujiulize*, *tuchukue*, na *tumeshiriki* katika hotuba hizi ilisaidia kuwafanya wananchi kuamini viongozi wao ni sehemu ya jamii na kwamba kweli wanaguswa na yale wanayoyaeleza. Hivyo, imani hiyo inahamasisha wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi ambayo ni miongoni mwa malengo ya viongozi wote. Matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yanaelezwa pia na Sovu (2021). Yeye anaeleza kwamba wagombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini Tanzania, wagombea wa uchaguzi walipendelea kutumia nafsi ya kwanza wingi ili kujikaribisha wao pamoja na jamii katika uungaji mkono wa sera za chama cha mgombea.

***c) Matumizi ya Nafsi ya Tatu***

Nafsi hii inawakilishwa na kiwakilishi nafsi ya tatu umoja {*yeye*}, kiambishi cha nafsi ya tatu umoja, kimilikishi nafsi ya tatu umoja {*-ke*}, kiwakilishi nafsi ya tatu wingi{wao}, kiambishi nafsi ya tatu wingi {*wa-*} na kimilikishi nafsi ya tatu wingi {*-o*} (Rubanza, 1996 na Hassan, 2021). Kwa kuzingatia data zilizokusanywa imebainika kwamba kiongozi hutumia nafsi ya tatu katika mtazamo hasi juu ya suala fulani. Lengo la matumizi ya nafsi ya tatu ni kuwafanya wanajamii wasikubaliane na mitazamo mingine inayoelezwa na viongozi pinzani. Pia, kama Michira (2014) anavyoeleza, nafsi ya tatu hutumika ili kukwepa kuwataja kwa majina wapinzani wao. Katika utafiti uliozaa makala haya, imebainika pia kwamba Rais William Samoei Ruto pia anatumia nafsi hii ili kujitofautisha na wapinzani ambao kwa mtazamo wake hawawezi kufanya vizuri kama yeye. Pia, pengine haoni sababu za kuwataja kwa majina kwa sababu atawapa umaarufu wa kisiasa usiostahili kwa wananchi. Tazama Data Na. (3).

Data Na. (3)

i. Wananchi wenyewe watajiamulia, kati ya mimi na **wale** nani anasema uongo.

**Chanzo**: Rais Dkt. William Samoei Ruto, kikao na waandishi wa Habari kuhusu Ziara katika Mlima Kenya

Data Na. (3) inaonesha matumizi ya nafsi ya tatu katika neno *wao*. Katika data hii tunaona kwamba kuna watu ambao ni kundi kinzani ambalo lina watu *wao* ambao wanatoa hoja kinzani. Katika data hii hana wasiwasi na tabia yake ya kuwa mkweli na ndiyo maana anasema "wananchi wataamua" kama anasema uongo wao wa kundi kinzani ndio wasemao uongo. Aidha, hawataji kwa majina kwa sababu za kisiasa. Kwa hiyo, Rais William Samoei Ruto ametumia kiwakilishi *wao* ili kuwashawishi wananchi kwamba yeye ni bora na wananchi waendelee kumuamini kuliko wapinzani wake.

***d) Matumizi ya Kauli Mbiu***

Kaulimbiu ni msemo ulio rahisi unaotumiwa na vyama vya siasa, mashirika au matangazo wenye kuwahamasisha watu kufuata wazo fulani (TUKI, 2019). Kwa kawaida, kauli mbinu hushawishi watu ili wafuate wazo fulani kwa sababu zinabeba ujumbe mzito kuhusu suala husika. Data zinaonesha kwamba matumizi ya kaulimbiu mbalimbali hulenga kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii ambayo yanaanzishwa au ni maono ya kiongozi ambaye katika makala haya ni Rais Samia Suluhu Hassan au Rais William Samoei Ruto. Aidha, wananchi wanapozisikia kaulimbiu hizo hupata ujumbe huo na hivyo kuhamasika kutekeleza jambo linalohamasishwa. Tazama Data Na. (4).

Data Na. (4):

i. Kuanzia Morogoro hadi Rukwa, Mwanza hadi Ruvuma na Zanzibar, kote niliona ***kazi inaendelea***.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. Aidha, tumetekeleza dhamira ya *kumtua mama ndoo kichwani*, kwa kusimamia utekelezaji wa miradi 1,300 ya maji nchi nzima.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

Data Na. (4) inaonesha matumizi ya kaulimbiu mbalimbali. Kauli mbiu hizi zinatumika kama nyenzo ya kutimiza malengo ya viongozi, yaani kuhamasisha na kushawishi watu kufanya kazi au kutumiza yale yanayosemwa na viongozi hao. Kwa mfano, kauli mbiu ya ***kazi inaendelea*** katika hotumba ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imebebe ujumbe kwamba licha ya vikwazo vyote kutokana na kifo cha hayati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, bado yale malengo yake na mambo aliyoyaanzisha yanaendelea kutekelezwa. Hivyo, kauli mbio hii inafanya wananchi kuwna kushwishika na kuamini zaidi malengo ya Rais Dkt. Samia Suhuhu Hassan. Pia, kaulimbiu ya ***kumtua mama ndoo kichwani*** katika hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan imebeba ujumbe kwamba serikali yake imedhamiria kumaliza tatizo la maji kwa Wanawake. Ujumbe huu unawafanya wananchi hao kumuamini kwamba anatatua matatizo yao na hata akiendelea kuongoza basi atatatua zaidi matatizo yao.

***e) Matumizi ya Maneno ya Lugha ya Kwanza***

Hii ni mbinu inayohusisha matumizi ya maneno ya lugha ya kwanza ya jamii inayohamasishwa kuhusu suala fulani. Data zinaonesha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto hutumia lugha hii wanapozungumza na wanajamii katika maeneo yao ya asili. Matumizi haya ya lugha ya kwanza huwafanya wanajamii waelewe suala linaloelezwa kwa undani. Pia, hufanya wanajamii hao wamuone kiongozi huyo kama mwanajamii mwenzao na hivyo kumuamini na kutekeleza kile anachowaambia. Data Na. (5) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (5):

i. Kibukusu (Kiluhya)

Omwa Yesu yichomiche! Mli moyo? Mlibaramu? Mwasangalile?

Bwana Yesu asifiwe! Mko wazima? Mko wazima? Mmefurahi?

**Chanzo**: Rais. Dkt. William Samoei Ruto akiwa Kanisani, Bungoma

ii. Kijaluo

Amoso u jo thurwa! Jothurwa untie? Jothurwa umor? Jothurwa uil?

Nawasalimu watu wote wa nyumbani! Watu wa nyumbani mpo? Watu wa nyumbani mna furaha? Watu wa nyumbani mmechangamka?

**Chanzo**: Rais. Dkt. William Samoei Ruto akiwa Kisumu

Data Na. (5) inaonesha namna Rais William Samoei Ruto akizungumza Kibukusu wakati akizungumza na jamii ya Wabukusu katika maeneo yao ya asili huko Bungoma. Pia, tunaona akizungumza Kijaluo wakati akizungumza na Wajaluo katika maeneo yao ya asili huko Kisumu. Rais Ruto ametumia mbinu hii ili kujinasibisha na jamii ya Wabukusu au Wajaluo. Matumizi haya ya lugha ya asili huwashawishi wananchi kumpenda na kumkubali kwa sababu wanaamini ni mmoja wao. Kwa hiyo, ni wazi kwamba Rais Ruto hutumia lugha kama nyenzo ya kutimiza malengo yake ya kuendelea kushika dola.

***f) Matumizi ya Nahau, Misemo, Methali na Tamathali za Semi***

Hivi ni vifungu vya maneno ambavyo vinabeba ujumbe mzito kuhusu suala linalohamasishwa. Lengo la matumizi ya vifungu hivi vya maneno ni kuwafanya wanajamii wapate ujumbe kwa namna inayowagusa na hatimaye kuhamasika kukubali au kukataa kushiriki. Data zinaonesha kwamba viongozi nchini Tanzania na Kenya hutumia vifungu hivi vya maneno ili kufikisha ujumbe kwa

namna ya mguso. Lengo lao ni kuwashawishi wanajamii ili waendelee kuwaamini katika uongozi wao. Data Na. (6) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (6):

i. Ndugu zangu, waswahili wanasema, ***usipojipangia, utapangiwa***.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kufungua Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050+, Dodoma, Disemba 9, 2023.

ii. Wengine wanasema ***ujinga ni wakati wa kwenda, wakati wa kurudi unakuwa umeshasoma umeshaerevuka***.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Januari 30, 2024.

iii. Kwa maneno mengine ***Msitoboe dau tunalosafiria*** ndani ya hilo dau tuko wote, ukitoboa yakiingia maji tukizama tunazama wote. Lakini pia labda niseme msiingie kwenye mtego wa ***kurarua nyuzi zilizounganisha kitambaa cha Taifa letu***.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Kongamano la Kongamano la Kitaifa la Maendeleo ya sekta ya habari tanzania na kikao kazi cha maafisa habari wa serikali tarehe, Juni 28, 2024.

Data Na. (6) inaonesha matumizi ya vifungu vya maneno ambavyo vinabeba ujumbe nzito. Mathalani, msemo wa ***usipojipanga utapagiwa*** katika hotuba hii unabeba ujumbe wa kwamba katika jambo lolote lile ni vema kufanya mwenyewe kuliko mtu mwingine akafanya kwa niaba yako. Kifungu hiki cha maneno kinawashawishi wananchi kwamba uongozi wa Rais Samia umaamini katika kufanya yenyewe bila kufanyiwa na watu kutoka mataifa mengine. Pia, ***ujinga ni wakati wa kwenda, wakati wa kurudi unakuwa umeshasoma umeshaerevuka*** katika hotuba hii imebeba ujumbe wa kwamba hata kama kuna makosa yanafanyika kwa mara ya kwanza, makosa hayo yanaweza kurekebishwa kwa awamu nyingine. Aidha, matumizi ya kifungu ***Msitoboe dau tunalosafiria*** hulenga kufikisha ujumbe kwamba Watanzania wasiharibu chochote kinachowanufaisha wote. Vilevile, kifungu cha ***tusirarue nyuzi zilizounganisha kitambaa cha Taifa letu*** kililenga kuhamasisha umoja wa Taifa la Tanzania. Kwa ujumla, vifungu hivi vyote vinashawishi wasikilizaji na kuona uongozi wake umejaa misingi ya kujitegemea, kujiamini, umoja na amani.

***g) Matumizi ya Istilahi Rasmi***

Hii ni aina ya lugha inayohusisha maneno rasmi yanayotumika katika ugha au mada fulani inayozungumziwa. Lengo lake ni kuaminisha wasikilizaji kwamba wanaelewa wanachozungumza na kwamba wawaamini yale wanachosema. Data zinaonesha kwamba Rais Samia na Rais Ruto hutumia istilahi rasmi zinazoendana na mada wanazozungumzia katika muktadha husika. Tazama Data Na. (7).

Data Na. (7)

i. Tukiangazia *miradi ya kimkakati*, baadhi yake tayari imefikia hatua ya kuanza kutoa huduma.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. Miongoni mwa mipango hiyo ni utekelezaji wa ***Mradi wa kielelezo*** ikiwemo ununuzi wa meli za kisasa za uvuvi katika Bahari Kuu

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Janiuari 30, 2024.

iii. Masuala ya **akili bandia**, **teknolojia ya sarafu za kidijitali** (crypto currencies) na hitajio la ***teknolojia ya nishati mbadala*** inaweza kuwa fursa au changamoto kwetu.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kufungua Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050+, Dodoma, Disemba 9, 2023.

Data Na. (7) inaonesha namna Rais Samia anavyotumia istilahi rasmi zinazoendana na mada. Kwa mfano, *miradi ya kimkakati*, *mradi wa kielelezo*, *akili bandia*, *sarafu za kidijitali*, na *nishati mbadala* ni istilahi rasmi. Matumizi ya istilahi hizi yalilenga kuwashawishi wasikilizaji kuamini kwamba anajua kile anachokiongea.

***h) Matumizi ya Lugha Isiyo Rasmi***

Data zinaonesha kwamba viongozi nchini Tanzania na Kenya hutumia lugha isiyo rasmi wanapozungumza na wananchi wao kulingana na kundi linalohusika. Lengo la kutumia lugha hiyo ni kuwashawishi wananchi hao kwa njia ya kuninasibisha nao ili wawaone kama nao ni sehemu ya kundi lao au wanajua mambo yao. Data Na. (8) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (8)

i. Kama nilivyosema, mkopo huu sio ***kaushadamu***, ni mkopo ambao unafanya kazi unalipa kilekile ulichokopeshwa.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Januari 30, 2024.

Katika Data Na. (8) tunaona kwamba Rais Samia anatumia maneno *kaushadamu* kurejelea aina ya mkopo wenye riba kubwa wakati anazungumza na wananchi katika halfa ya kukabidhi boti za wavuvi. Alitumia lugha hiyo huku akiamini kwamba anazungumza na kundi ambalo wao wanelewa lugha hiyo kuliko ingekuwa lugha rasmi. Lengo lake hapa ni kujinasibisha kwa kuwaaminisha wananchi anaozungumza nao kwamba anafahamu aina hiyo ya mkopo na kwamba serikali yake haiafiki aina hiyo ya mkopo. Aidha, badala yake serikali inatoa mkopo rafiki kabisa kwa kuzingatia mapato ya mkopaji. Lugha hii inawashawishi wananchi na kuendelea kumpenda na kumkubali Rais wao.

***i) Matumizi ya Lugha ya Kitakwimu***

Hii ni lugha ya ushahidi kwa kutumia data kuhusu utendekaji wa suala linalozungumziwa. Data zinaonesha kwamba viongozi hutumia lugha hii katika muktadha ambao hutoa data juu ya utokeaji wa jambo hilo. Lengo la matumizi ya lugha hii ni kuwahasisha wananchi suala linaloelezwa kwa kuwaonesha ukweli halisi wa utokeaji wa suala hilo. Tazama Data Na. (9).

Data Na. (9)

i. Kati ya Januari hadi Juni 2024 uchumi ulikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. Kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kati ya Januari hadi Novemba 2024, tumesajili miradi ya uwekezaji 865 yenye thamani ya Dola za kimarekani bilioni 7.7 inayotarajia kuzalisha ajira 205,000.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

iii. Kwa upande wa mapato, Mamlaka ya ukusanyaji Mapato Tanzania (TRA) imefanikiwa kukusanya Shilingi trilioni 21.276 kati ya mwezi Januari na Oktoba, 2024 sawa na asilimia 99.3 ya lengo. Hili ni ongezeko la asilimia 17.5 ikilinganishwa na makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

Data Na. (9) inaonesha matumizi ya takwimu katika hotuba ya Rais Samia. Kwa mfano, tofauti ya asilimiaa 5.4% na asilimia 4.8% ilitumika ili kuonesha ni kwa namna gani Uchumi wa Tanzania umekuwa katika vipindi viwili tofauti. Takwimu hii inamshawishi mwananchi aamini kwamba uongozi wake unafanya vizuri na kwamba akiendelea zaidi Uchumi utakuwa zaidi. Hivyo, ni wazi kwamba matumizi ya takwimuyanamwamisha mwanananchi na hivyo kuna uwezekano mkubwa sana wa Rais huyu kuendelea kuongoza Tanzania pindi atakapoomba ridhaa yao tena.

***j) Matumizi ya Lugha ya Ushirikiano***

Hii ni lugha inayodokeza ushirikiano wa viongozi na wananchi wanaowaongoza. Lugha hutumika ili kushawishi wananchi kwamba uongozi wao haujichukulii maamuzi bila kushirikisha wananchi wake. Lugha hii inatumika kama nyenzo ya ushawishi kwa sababu inapotumika huwaaminisha wananchi kwamba wao ni sehemu ya nchi, wao ni sehemu ya maamuzi na maono ya kiongozi huyo. Tazama Data Na. (10).

Data Na. (10)

i. Hapa nataka nisisitize kuwa, miradi hii ni ***yetu sote***, na imejengwa kwa kutumia ***rasilimali zetu***. Hivyo, *tunawajibika kuitunza* ili ***itunufaishe sisi na vizazi vijavyo*** kesho**.**

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. ***Tulisimama pamoja kama Taifa***, misaada ya kibinadamu kwa waathirika kama vile vifaa vya ujenzi, chakula, nguo na malazi ilitolewa.

Chanzo: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

iii. Tunaendelea kuwakaribisha kwa ***mashirikiano*** zaidi kwenye sekta hii muhimu… Kama mtakwamwa, Waziri unajua kwamba ***milango yangu iko wazi***, njoo ***tushauriane***, na mtendaji wako tuone tunalipeleka vipi jahazi hili.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Janiuari 30, 2024.

Data Na. (10) inaonesha kwamba Rais Samia anatumia lugha ya *rasilimali zetu*, *tulisimama pamoja kama taifa* na *milango yangu iko wazi njoo tushauriane*. Maneno *rasilimali zetu* yanapotumika huwafanya wananchi waone kwamba hata wao ni sehemu ya rasilimali za nchi. Aidha, *maneno tulisimama pamoja kama taifa* huwafariji wananchi na kujiona kwamba nao hushirikiana na Rais katika kutatua changamoto za nchi. Vilevile, maneno *milango yangu iko wazi njoo tushauriane* huaminisha kwamba Rais Samia anafikika na ni msikivu na wala hafanyi maamuzi ya kwake peke yake. Kwa ujumla, lugha ya ushirikiano inapotumika huwashawishi wananchi na kuona kwamba uongozi wa Rais Samia ni shirikishi.

***k) Matumizi ya Lugha ya Kujiamini***

Lugha hujumuisha matumizi ya maneno au sentensi yanayodhihirisha uwezo wa kiongozi. Lengo la matumizi ya lugha hii ni kudhihirisha uwezo wa utendajikazi wa kiongozi kwamba wanaweza kuongoza. Data zinaonesha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto hutumia aina hii ya lugha ili kuaminisha wananchi kwamba wanaweza na kwamba hakuna linaloshindikana kwao. Data Na. (11) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (11)

i. ***Serikali imejipanga*** kikamilifu kuchochea ukuaji wa Sekta ya Uvuvi kupitia Mipango na Programu mbalimbali ili kuongeza mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Janiuari 30, 2024.

Data Na. (11) inaonesha kwamba matumizi ya maneno *serikali imejipanga* yanashawishi wananchi kwa kuwaaminisha kwamba serikali ya Rais Samia ina uwezo wa kuchochea ukuaji wa sekta ya uchumi kwa kutumia mipango yake mbalimbali. Wananchi wanaposikia maneno haya wanaendelea kumuamini Rais wao kwa sababu anauwezo mkubwa na ana mipango ya kutosha.

***l) Matumizi ya Lugha ya Matumaini***

Lugha hii hujumuisha matumizi ya maneno ambayo yanajenga Imani ya kutokea au kukamilika kwa jambo fulani lililoanzishwa au litakaloanzishwa. Lengo la matumizi ya lugha hii ni kuwashawishi wananchi kwamba wasikate tamaa na waendelee kujenga Imani kuhusu jambo linalotarajiwa kuanzishwa, kutokea au kukamilika. Data zinaonesha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto hutumia aina hii ya lugha. Aidha, lugha hiyo hujumuisha vitenzi kama vile tutaendelea, tutachochea, tutatoa, tunatazamia, tutakamilisha, inatarajiwa, imedhamiria, tunakwenda, tunaweza na tunatarajia. Kimofolojia, vitenzi hivyo huashiriwa na kiambishi cha wakati ujao {-ta-}. Tazama Data Na. (12).

Data Na. (12)

i. ***Tutaendelea*** kukamilisha miradi ya kimkakati, ikiwemo Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, Daraja la Kigongo/Busisi ambalo limefikia asilimia 94, linalotazamiwa kulikamilisha mwezi Februari, 2025. ***Tutatoa*** kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa kama vile Jiji la

Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma na kurahisisha usafiri na usafirishaji katika miji inayokua kwa kasi.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. Kwa madeni yaliyokwishafanyiwa uhakiki na yanalipika, ***niwaahidi*** kwamba ***tunakwenda*** kuyalipa.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Kongamano la Kongamano la Kitaifa la Maendeleo ya sekta ya habari tanzania na kikao kazi cha maafisa habari wa serikali tarehe, Juni 28, 2024.

Data Na. (12) inaonesha matumizi ya vitenzi vya matumaini kama vile *tutaendela*, *tutatoa*, *niwaahidi* na *tunakwenda*. Vitenzi tutaendelea na tutatoa vinadokezatumainisha kwamba miradi ya kimkakati na ile ya kupunguza msongamano ni miradi ambayo itakamilika katika wakati unaokuja yaani baada ya huo mwaka 2024. Aidha, vitenzi niwaahidi na tunakwenda vinatumainisha kwamba madeni yanayodaiwa bila shaka yatakamilika baada ya mwaka 2024. Wananchi walivyosikia lugha hii ya matumaini walishawishika kwamba serikali ya Dkt. Samia ni sikivu na kwamba itakamilisha mipango na ahadi walizotoa kwa wananchi. Kutokana na ushawishi huu, bila shaka atapata ridhaa ya wananchi pindi atakapoomba ridhaa yao kuendela kuongoza katika kipindi kijacho.

***m) Matumizi ya Lugha ya Haki***

Lugha hii hujumuisha matumizi ya maneno au sentensi zisizo na chembechembe zozote za dhuluma na kwamba kila mtu ana nafasi ya kupata kile anachostahili. Data zinaonesha kwamba Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto hutumia lugha chanya inayoonesha haki za wananchi wao. Lengo lao ni kuwashawishi wananchi kwamba wao ni wapenda haki na kwamba hawawezi kudhulumu mwananchi yeyote yule. Data Na. (13) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (13)

i. Biblia katika Mithali Sura ya 14, Mstari wa 34 na ametaja mmoja wetu hapa, inasema ***Haki huinua Taifa***. Kwa upande wa dini ya Kiislam, tunaambiwa, ***kwenye haki usisimamishe batili na kwenye batili haki haisimami***.

**Chazo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba ya maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini Tanzania, Februari 2, 2024.

Data Na. (13) inaonesha matumizi ya lugha ya haki kwa kuzingatia misingi ya kiimani. Matumizi ya maneno *haki huinua taifa* humaanisha kwamba taifa ambalo hakuna dhuluma basi taifa hilo linaendelea. Pia, matumizi ya maneno *kwenye haki usisimamishe batili na kwenye batili haki* humaainisha kwamba kila mtu mwenye haki apewe haki yake na si kinyume chake. Kwa ujumla, maneno haya huwashawishi wananchi na kuamini kwamba Rais Samia ni Rais anayeongoza kwa kutumia misingi ya haki. Kwa hiyo, wataendelea kumpenda na hata akiomba ridhaa tena bila shaka atachaguliwa tena na kuendelea kuongoza katika kipindi kijancho.

***n) Lugha ya Motisha***

Lugha hii hujumuisha matumizi ya maneno au sentensi zenye kutia moyo baada ya kufanya jambo fulani. Data zinaonesha kwamba viongozi hutumia maneno na sentensi za kuonesha pongezi au kushukuru ili kuwapa motisha wananchi wao. Lengo lake ni kuwashawishi wananchi waendelee kuwaamini na kufanya kile wanachowaelekeza. Tazama Data Na. (14).

Data Na. (14)

i. Kwa hakika, ***ninavipongeza*** vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulinda nchi yetu.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

ii. ***Ninawashukuru*** sana wananchi wote kwa ustahimilivu, **ushirikiano** na uelewa wenu tunapopatwa na changamoto za aina hio.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024

Data Na. (14i) inaonesha matumizi ya neno *ninavipongeza* wakati Rais Samia akitoa pongezi kwa vyombo vya ulinzi na usalama nchini Tanzani kwa kulinda nchi kwa mwaka 2024. Alitumia lugha hii ili kuvipa motisha vyombo hivyo ili wananchi waendelee kuwa salama na kumuamini zaidi. Data Na.

(14ii) inaonesha matumizi ya maneno *ninawashukuru* na *ushirikiano*. Rais Samia alitumia maneno haya ili kutoa shukrani na kwa wananchi wake kwa namna ambavyo wanavumilia na kuelewa changamoto mbalimbali. Ametumia lugha hii ili kuwapa motisha wananchi kwamba waendelee kuwa wavumilivu. Lugha hii haiwapi motisha tu bali inawashawishi kumuona Rais wao ni mtu aliyejaa shukrani.

***o) Lugha ya Kiimani***

Lugha hii hujumuisha matumizi ya maneno, sentensi au vifungu vya kiimani ya Kiisilamu au Kikristo. Imebainika kwamba viongozi hutumia lugha hii kuwashawishi wananchi wao kwambwa hata wao wanaongoza kwa kuzingatia misingi ya kiimani. Data Na. (15) inathibitisha hoja hii.

Data Na. (15)

i. ***Biblia katika Mithali Sura ya 14, Mstari wa 34*** na ametaja mmoja wetu hapa, inasema Haki huinua Taifa. Kwa upande wa dini ya Kiislam, tunaambiwa, kwenye haki usisimamishe batili na kwenye batili haki haisimami.

**Chazo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hotuba ya maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini Tanzania, Februari 2, 2024.

ii. Hata hivyo, kwa ***mapenzi ya Mwenyezi Mungu***, Mheshimiwa Ndugulile alituacha kabla hata ya kuingia ofisini. Tunazidi kumuombea pumziko la Amani.

**Chanzo**: Dkt. Samia Suluhu Hassan katika salamu za kuukaribisha mwaka 2025, Disemba 31, 2024.

iii. ***Imani*** ya Serikali ni kwamba mpango 26 huu utaongeza kasi ya kukuza vijana wafanyabiashara wapya kwenye sekta hii ya uvuvi na ***In shaa Allah***, watapatikana.

**Chanzo**: Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika hafla ya kukabidhi boti za uvuvi na vizimba vya kufugia Samaki huko Mwanza, Janiuari 30, 2024.

Data Na. (15) inaonesha matumizi ya maneno ya kiimani kama vile *Biblia katika Mithali Sura ya 14, Mstari wa 34, kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu*, *Imani*, *na In shaa Allah.* Rais Samia alitumia vifungu hivi ili kuwashawishi wananchi kwamba yeye anaamini katika misingi ya kiimani ya Kikristo au Uisilamu na kwamba hawezi kufanya kinyume na misingi hiyo. Aina hii ya lugha kuwafanya wananchi waendelee kumuamini kwamba uongozi wake umejaa misingi mizuri ya kiimani. Kuendelea kumuamini kunadokeza kwamba hata akiomba ridhaa yao tena watakuwa tayari kumchagua yeye kuliko atakaoshindana nao.

## Hitimisho

Kwa ujumla, makala haya yamechanganua lugha kama nyenzo itumiwayo na viongozi ili kutimiza malengo yao nchini Tanzania na Kenya. Makala imefafanua kwamba katika wakati huu wenye ushindani wa kisiasa na migogoro ya kiitikadi Rais Samia Suluhu Hassan na Rais William Samoei Ruto wameonekana kutumia aina ya lugha chanya ambayo inalenga kuwashawishi wananchi wako ili waendelee kushika dola. Lugha hiyo chanya inajumuisha matumizi ya: nafsi, kauli mbiu, lugha za kikabila, vifungu vya maneno kama vile misemo, methali na nahau. Vilevile, lugha hiyo inahusisha matumizi ya istilahi rasmi, istilahi isiyo rasmi rasmi na takwimu. Pia, imebainika kwamba wanatumia lugha ya ushirikiano, ya kujiamini, ya motisha, ya kutumisha na lugha ya kiimani. Imebainika kwamba lugha hii inashawishi wananchi kwa namna ya kujikubalisha na kujinasibisha na wanaowaongoza, kuwahamasisha, kuwaaminisha, kuwatumainisha, kuwaunganisha na kuwapa motisha. Kwa ujumla, viongozi tajwa ni mahiri na hodari wa matumizi ya lugha chanya ili kutimiza malengo yao.

## Marejeleo


Abdul, A. (2022). Legal and Political Intervention on Language Issues in Bangladesh: A Sociolinguistic Perspective. *Indonesian Journal of Sustainability, 1*(2), 22-35.

Abuya, E. J. (2012). A Pragma-Stylistic Analysis of President Goodluck Ebele Jonathan's Inaugural Speech. *English Language Teaching. Canadian Center of Science and Education, 5*(11).

Kurmanova, A., Sarsikeyeva, G., & Utegulova, G. (2021). Political Linguistics: Public Speech of American and Kazakh Politicians. *International Journal of Society, Culture & Language*, *9*(2), 212-221.

Ahmed, A. M. (2013). *Amar dekha rajnitir panchash bachhar* [Fifty Years of Politics as I Saw It]. Khoshroz Kitab Mahal.

Akinkurolere, S. O. (2011). *A Speech Act Analysis of Selected Political Speeches of President Umaru Musa Yar'adua*. An Unpublished M. A. Thesis of Department of English, Obafemi Awolowo University, Ile Ife.

Atkinson, J. M. (1983). Two Devices for Generating Audience Approval: A Comparative Study of Public Discourse and Text. In K. Ehlich and H. van Riemsdijk (Eds.), *Connectedness in Sentence, Text and Discourse* [199-236). Tilburg: Tilburg Papers in Linguistics.

Austin, J. L. (1962). *How to Do Things with Words*. London: Oxford University Press.

Ayeomoni, O. M., & Akinkuolere, S. O. (2012). A Pragmatic Analysis of Victory and Inaugural Speeches of President Umaru Musa Yar'Adua. *Theory and Practice in Language Studies, 2*(3), 461-468.

Balogun, S. (2015). *A Linguistic Stylistic Analysis of Parallelism in Inaugural Speeches of Presidents Barrack Obama and Goodluck Jonathan*. An unpublished Master's Thesis of the Department of English, Ahmadu BelloUnviersity, Zaria.

Beard, A. (2000). *The Language of Politics*. London: Rutledge.

Bell, D. (1988). Political Linguistics and International Negotiations. *Negotiations Journal, 4*(3), 233–46.

Bizzell, P., & Herzberg, B. (1990). *The Rhetorical Tradition: Readings from Classical Times to the Present*. Boston: Bedford.

Bugarski, R. (2004). Language Policies in the Successor States of Former Yugoslavia. *Journal of Language and Politics, 3*(2), 198–207.

Bull, P., & Fetzer, A. (2006). 'Who Are We and Who Are You? The Strategic Use of Forms of Address in Political Interviews. *Text and Talk, 26*(1), 1-35.

Carver, T., & Pikalo, J. (2008). Political Language and Metaphor: Interpreting and Changing the World.

Chilton, P., & Schaffner, C. (1997). *Discourse and Politics. Discourse as Social Interaction*, ed. by Teun van Dijk, 206–30. London: Sage.

Chilton, P. (1998). Politics and Language. *Concise Encyclopaedia of Pragmatics*, 688-694. London: Elsevier.

Chilton, P. (2004). *Analysing Political Discourse: Theory and Practice*. London: Routledge.

Cuddon, A. (2015). *The Penguin Dictionary of Literary terms and Literary Theory*. London: The Penguin Group.

Dallmayr, F. (1984). *Language and Politics: Why Does Language Matter to Political Philosophy*. London: University of Notre Dame.

Degani, M. (2018). From the Light of Truth to the Dark Alleys of Tyranny: The Evocative Power of Metaphor in American Political Speeches. *Metaphor and the Social World, 8*(2), 157–183.

Fairclough, N. (2000). *New Labour, New Language*. London: Routledge.

Gastil, J. (1992). Undemocratic Discourse: A Review of Theory and Research on Political Discourse. *Discourse & Society, 3*(4), 469-500.

Hager, A., & Hilbig, H. (2020). Does Public Opinion Affect Political Speech? *American Journal of Political Science, 64*(4), 921–937.

Heritage, J., & Greatbatch, D. (1986). Generating Applause: A Study of Rhetoric and Response at Party Political Conferences. *American Journal of Sociology, 92*, 110-157.

Hudson, K. (1978). *The Language of Modern Politics*. London: MacMillan.

Helmbrecht, J. (2002). Grammar and Function of 'We'. In A. Duszak (Ed.), *Us and Others* [31-50]. Amsterdam: Benjamins.

Ismailov, F., Rayeva, G., Koblanova, A., Yelikbayev, B., & Yessenova, K. (2020). Analysis of Political and Diplomatic Language in Linguistic, Cognitive and Pragmatic Aspects, *Opción, Año 36*(91), 803-819.

Iwamoto, N. (2005). The Role of Language in Advancing Nationalism, Political Science, Linguistic Journal.

Kaur, P., & Shapii, A. (2018). Language and Nationalism in Malaysia: A Language Policy Perspective. *International Journal of Law, Government and Communication, 3*(7), 1-10.

Kövecses, Z. (2002). *Metaphor: A Practical Introduction*. Oxford: Oxford University Press.

Kramsch, C. (2009). *Language and Culture*. London: Oxford University Press.

Lakoff, R. (1990). Talking power. Basic Books.

Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). Metaphor We Live By. Chicago: University of Chicago Press.

Lin, D. (2019). *A Contrastive Study of University English-Medium Instruction Lectures Given by Native and Non-Native English Lecturers: Rhetorical Move Structure and Formulaic Language*. [PhD Dissertation]. School of Foreign Languages Institute of the Social Technology Suranaree University of Technology.

Lopez, A. (2000). *Targeting Media*. Sydney: Copyright Agency Limited.

Lum, C. (2002). *Scientific Thinking in Speech and Language Therapy*. New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates, Inc.

Macagno, F., & Walton, D. (2014). *Emotive Language in Argumentation*. New York: Cambridge University Press.

Maitland, K., & Wilson, J. (1987). Ideological Conflict and Pronominal Resolution. *Journal of Pragmatics, 11*, 495-512.

Markowitz, D. M., & Slovic, P. (2020). Communicating Imperatives Requires Psychological Closeness but Creates Psychological Distance. *Journal of Language and Social Psychology, 39*(5– 6), 598–625.

Mendal, N. (2001). *Language and Politics, Political Theory and Practice*. The University of British Comumbia.

Michira, J. (2014). The Language of Politics: A CDA of the 2013 Kenyan Presidential Campaign Discourse. *International Journal of Education and Research, 2*(1), 1-18.

Nick, S. (2001). Language in Diplomacy. *Language in Diplomacy* (39). University of Malta.

Opeibi, B. O. (2009). *Discourse, Politics and the 1993 Presidential Election Campaigns in Nigeria*. Lagos: Nouvele Communications Limited.

Pelinka, A. (2007). Language as a Political Category: The Viewpoint of Political Science. *Journal of Language & Politics*, *6*(1), 129–43.

Şeker, N. (2005). Identity Formation and the Political Power in the Late Ottoman Empire and Early Turkish Republic. *HAOL, 8*(Otoño), 59-67.

Scotto Di Carlo, G. (2020). The 'Trumpusconi' Phenomenon: A Comparative Discourse Analysis of US President Trump's and Former Italian Prime Minister Berlusconi's Political Speeches. *International Journal of Language Studies, 14*(2), 43–72.

Schaffner, C. (1996). Editorial: Political Speeches and Discourse Analysis. *Current Issues in Language and Society, 3*(3) http://pdfserve.informaworld.com/

Searle, J. R. (1969). *Speech Acts: An Essay in the Philosophy of Language*. Cambridge: CU.

Shah, S. W. A., & Pathan, H. (2016). Representation of Western Culture in O' Level English Language Textbooks. English Language Forum (ELF), 18.

Sovu, Y. A. (2020). *Uchanganuzi wa Mbinu za Kisarufi na za Kibalagha katika Vilongo Teule vya Kampeni za Uchaguzi wa Mwaka 2015, Nchini Tanzania*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sovu, Y. A. (2021). Uchanganuzi wa Mbinu za Kisarufi katika Kampeni za Uchaguzi: Mifano Kutoka katika Uchaguzi Mkuu wa Tanzania Mwaka 2015. *CHALUFAKITA*, *3*(1), 121-141.

Tanaka, K. (1992). *Kokkago o Koete* [Beyond a National Language]. Tokyo: Chikuma Publishing Co.

Tong, H. K., & Cheung, L. H. (2011). Cultural Identity and Language: A Proposed Framework for Cultural Globalization and Glocalization. *Journal of Multilingual and Multicultural Development, 32*(1), 55-69.

TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Toleo la 4. Dar es Salaam: TUKI

VIDE-MUWA. (2018). Kamusi Kuu ya Kiswahili

Wilson, J. (1990). *Politically Speaking*. Basil Blackwell.

Xhemaili, M. (2022). The Importance of The English Language in Public Diplomacy and International Relations. *Journal of Liberty and International Affairs*. DOI: https://www.doi.org/10.47305/JLIA2281322x